Misri na Uganda

Mkuu wa Bodi ya Wakurugenzi

Diaa Rashwan

Mwandishi

Abdelmoeti Abouzaid

Mkuu wa Sekta ya Vyombo vya Habari za Nje

Kimefasiriwa na :

Asmaa Elsayed Belal

Basant Khaled

Enas Ebrahim

Lailaa Alaa Eldeen

Kimerejewa na :

Issa Ramadhani Majilanga

Utoaji wa kisanaa:

M/ Rania Saleh

Ganda :

Abeer Ahmed

Msimamizi wa Uchapichaji

M/Iman gaafar

Kimechapishwa na

Mamlaka Kuu ya Habari

3, Barabara ya Al-Estad Al-Bahary-Mji wa Nasr -Kairo

Simu :002 02 22616716

Fax.: 002 02 22608444

Barua Pepe:
african_perspectives@yahoo.com

Site Internet :

africa.sis.gov.eg

KAIRO

2019

Toleo hili linasambazwa bure

na haliuzwi

w

Yaliyomo

utangulizi

Mfululizo huu:.....5

Kitabu hiki :.....7

Sura ya kwanza: Historia na maendeleo ya mahusiano kati ya Misri na Uganda.....9

Sura ya pili: Mahusiano ya kisiasa 11

Sura ya tatu: Mahusiano ya kiuchumi 19

Sura ya nne: Ushirikiano kati ya Misri na Uganda kuhusu maji ya Mto wa Nile……..……..... 25

Mfululizo huu::

Uenyekiti wa Misri kwa Umoja wa Afrika kwa mwaka wa 2019 ni kama kuthamini undugu wa nchi za Afrika, na kuiamini Misri na Rais wake, Rais Abdel Fattah Al-Sisi.

Nchi ya Misri, katika ngazi zote, inafanya kazi hii kama heshima, jukumu na wajibu wa kutimiza ili kuhakikisha manufaa kwa bara la ww na kukuza ushirikiano kati ya raia wake.

Mamlaka kuu ya habari ilianzisha mfululizo wa shughuli katika nyanja za vyombo vya habari mubashara (moja kwa moja) kielektroniki na kuchapishwa, na hayo ilikuja kama sehemu ya jukumu lake kama taasisi ya habari ya umma ya kimisri.

Miongoni mwa shughuli hizi ni mfululizo wa vitabu ambavyo vinachapishwa katika karatasi na kwenye tovuti za Mamlaka kuu ya habari.

Mfululizo huo ulianza na kitabu kinachoitwa «Misri katika Afrika», kilichofuatiwa na vitabu kadhaa, kila kitabu kinazungumzia nchi za Afrika na uhusiano wake na Misri, ili kukuza ushirikiano kati ya raia wa Afrika, kuimarisha ujuzi wa raia wa Misri kuhusu ndugu zao wa nchi za Afrika na kuzungumza na raia wa Afrika kwa lugha zao.

Kitabu hiki:

mahusiano ya kale ya Kijiografia, kihistoria, rasmi na Misri na Uganda zina kienyeji kwa muda mrefu sana. Mto wa Nile ni ateri (mshipa mkuu) wa maisha unaounganisha kati ya nchi hizo mbili, ambapo mawasiliano ya kistaarabu na kibinadamu kati ya nchi za Bonde la Nile yamekua na kuendelea juu ya pande zake mbili . Katika zama za sasa , Misri na Jamhuri ya Uganda zimekuwa na mahusiano yenye nguvu yanayorejea katika kipindi cha ushirikiano kwa ajili ya kutafuta uhuru kutoka kwa ukoloni wa kigeni.

Kisha ushirikiano huu umeendelea katika vipindi vifuatavyo kutokana na umuhimu wa mahusiano hayo kwa nchi hizi mbili, na kwa ajili ya utulivu katika Afrika ya Mashariki na Bara kwa ujumla, Kulingana na hali na jukumu la kila mmoja katika mazingira yake ya kikanda na ya bara.

Misri ina nafasi yake muhimu katika ulimwengu wa Kiarabu , Mashariki ya Kati na Afrika, na Uganda ina jukumu muhimu katika ngazi ya udhibiti wa bara (Umoja wa Afrika), au mashirika saidizi ya kikanda, nayo ni moja wapo ya nchi za Bonde la Nile, ambayo ina uhusiano wa nguvu na nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika.

Katika miaka ya hivi karibuni. Mahusiano ya Misri na Uganda yamepata nguvu zaidi, hasa kupitia kufanya mikutano sita kati ya Marais wawili, Abdul Fattah Sisi na Yoweri Museveni kupitia ziara ya Rais Sisi kwenda Uganda mwaka 2016 na 2017, ziara ya Rais Museveni kwenda Misri mwaka 2018, pia ilifanyika mikutano mitatu wakati wa ushiriki wao katika kikao cha 96 cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa huko New York mwaka 2014, na katika mikutano miwili ya Umoja wa Afrika huko Malabo mwaka 2014 na Addis Ababa mwaka 2015. Na mwaka 2016, utaratibu wa mawasiliano ya kisiasa kati ya nchi hizo mbili yalianzishwa na ilifanyika ziara yake ya kwanza Mei 2018.

Nchi hizo mbili zinaendelea kuimarisha uhusiano wao wa nchi mbili katika maeneo ya kisiasa na kiuchumi na maji ya Nile, kupambana na ugaidi na yote ambayo yanahakikisha maslahi ya wananchi wao na bara la Afrika.

Sura ya kwanza

Maendeleo ya mahusiano kati ya Misri na Uganda

kuna mahusiano ya kihistoria kati ya Misri na Uganda tangu zama za kale kwa sababu ya mawasiliano baina ya wanachi wa Bonde la mto Nile, na wakati wa Khedewi Ismail bin Ibrahim bin Mohammad Ali alipotawala Misri , alitaka kuhifadhi vyanzo vya kitropiki vya Mto Nile, hasa ziwa kubwa la nyanza (viktoria) na utawala wake ulikuwa umeenea hadi Kusini mwa Sudan , Mfalme huyu aliipa umuhimu mkubwa sana Uganda kwa sababu ya umuhimu wake wa kimkakati kwani vyanzo vya Mto Nile vinaanzia nchi hii, na alituma majumbe wake kwa Wafalme wa Uganda, aidha utawala wa Othmani uliacha pwani ya magharibi ya bahari ya Shamu na pwani ya ghuba ya Aden, na kukaribishwa na Wafalme wa Uganda kwa jambo hilo.

Kisha Misri chini ya uongozi wa Rais Gamal Abdel Nasser, ilisaidia mapambano ya watu wa Uganda kwa ajili ya ukombozi kutoka utawala wa Waingereza.

baada ya uhuru , Milton Obote , aliomba msaada wa Misri kukabiliana na wapiganaji wa Congo wenya silaha, waliovuka mipaka ya Uganda chini ya uongozi wa “Tshombe.”

Rais Gamal Abdel Nasser aliamua kutuma nusu ya kikosi cha ndege cha Misri MiG-17 kwa ajili ya kusaidia Uganda, pia ametoa amri kwa wataalumu katika nchi hizo mbili kufanya mipangilio na kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa azimio hili na kabla ya na kabla ya mipango kukamilika, balozi wa Misri huko Kampala alituma Telegram ili kusisitiza kwamba uadui kwenye mipaka ya Uganda umesimama kabisa.

Na kwamba kujibu kwa haraka kwa Rais Gamal Abdel Nasser na habari za jibu hili kwa Tchombe, ilikuwa ni sababu kuu ya kusimamisha uadui kabisa kwenye mipaka ya Uganda.

na kuunga mkono msimamo imara wa wananchi wa Uganda dhidi ya vishio vya Tchombe.

Katika miongo iliyofuata, hasa baada ya Rais Yoweri Museveni kuchukua mamlaka nchini Uganda Mwezi wa januari 1986, mahusiano baina ya nchi hizo mbili yaliendelezwa na kuimarishwa katika nyanja mbalimbali hasa ushirikiano kuhusu Mto wa Nile, nyanja ya ushirikiano wa kifundi na usimamizi wa rasilimali za vyanzo vya maji kwa ujumla, aidha nchi hizo mbili zinashirikiana katika juhudi za kuhakikisha amani na utulivu katika Afrika ya Mashariki na eneo la pembe ya Afrika.

kwa pande wa mahusiano baina ya nchi hizo mbili , ushirikiano wa kifundi umeimarishwa kwa ajili ya maendeleo, kuandaa makada na mafunzo, pia nchi hizo mbili zimeshiriki katika uanachama wa mashirika kadhaa na makundi mengi hasa muungano wa soko la pamoja la mashariki na kusini la afrika COMESA.

jambo ambalo limesaidia uhuru wa biashara kati ya nchi wanachama, na juhudi hizo izimefanya kuboresha ushirikiano wa biashara na ushirikiano wa uwekezaji baina ya nchi hizi mbili, ingawa bado kufikiwa kiwango cha uwiano ambao unalingana na mahusiano ya kisiasa baina nchi hizo mbili.

katika miaka ya hivi karibuni,nchi ya Uganda imeiunga mkono Misri katika umoja wa Afrika baada ya mapinduzi ya Juni 30.

sura ya pili:
mahusiano ya kisiasa

kwa zaidi ya miaka 30 nchi mbili za Misri na Uganda zimeonesha azma ya pamoja ya ushirikiano kuhusu pande kadhaa za mahusiano ya kisiasa na kiuchumi, pia kuhusu masuala ya kieneo hasa sudani ya kusini na eneo la pembe ya afrika.

na kuhusiana na Mto Nile , ushirikiano wa kifundi katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa ujumla , ushirikiano wa kijeshi , kukabiliana na tisho la ugaidi pamoja na ushirikiano wa usalama na ajenda ya maendeleo katika bara la afrika.

Rekodi ya ziara na mikutano kati ya viongozi wa nchi hizo mbili , unaonesha maendeleo mazuri baina ya Misri na Uganda katika miaka ya hivi karibuni.

Katika kiwango cha Mkutano wa kilele:

Mkutano wa kwanza ulifanyika baina ya Rais Abdulfattah Alsisi na Rais Yoweri Museveni pembezoni mwa mkutano wa kilele wa Umoja wa Afrika huko Malabo,mji Mkuu wa Guinea Ikweta juni 2014.

Tarehe 23-9-2014 Raisi wa Misri Abdulfattah Alsisi alikutana na Rais wa Uganda Yoweri Musevenii pembezoni mwa shughuli za kikao cha sitini na tisa cha Baraza kuu la Umoja wa Mataifa. Pande hizo mbili zilijadili njia za kukuza ushirikiano katika nyanja mbalimbali baina ya nchi hizo mbili , Marais wawili walikubaliana umuhimu wa kufaidika kwa maji ya Mto Nile na kufikia malengo ya maendeleo kwa ajili ya maslahi ya raia wa bara la Afrika bila ya kusababisha madhara kwa maslahi ya upande yoyote.

mkutano wa tatu baina ya Marais wawili ulifanyika wakati wa mkutano wa Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa , mwezi wa januari 2015.

katika mwezi wa Desemba 2016, Raisi Abdulfattah Alsisi alikwenda kwa mara ya kwanza nchini Uganda , ziara hii ilisisitiza kuwepo mahusiano ya kihistoria tangu karne nyingi zilizopita , jambo ambalo linazingatiwa kuwa ni hatua ya kwanza mpya ya kuwepo mahusiano na umuhimu wa kuamsha shughuli za tume ya pamoja kati nchi mbili , na umuhimu wa kufanikiwa katika nafasi ya kwanza .imesisitizwa kwamba Misri ina nia ya kuimarisha mazungumzo na Uganda kuhusu masuala mbalimbali ya Kikanda.

Rais wa Uganda pia amesisitiza umuhimu wa kuimarisha mazungumzo na ushirikiano baina ya nchi za bonde la Mto Nile, akiashiria kwamba ana nia ya kufikia jambo hilo kupitia muda wa uongozi wake wa mpango wa nchi za bonde la Mto Nile , pia Marais wawili wameonesha uhusiano wao kuhusu mradi wa unganisho la Bahari kati ya Ziwa viktoria na Bahari ya Mediterane, Marais wawili wamesisitiza kwamba umuhimu wa kuchukua hatua ya lazima kutekeleza mradi huo ,baada ya kumaliza utafiti wake ,pia katika ziara hiyo ilitiwa saini ya mfumo wa ushauriano wa kisiasa kati ya nchi mbili.

Tarehe 21-6-2017, Rais wa Misri Abdulfattah Alsisi alikwenda Uganda ili kushiriki katika shughuli za mkutano wa nchi za bonde la Mto nile, Raisi wa Uganda alimpokea na wamefanya mazungumzo muhimu pembezoni mwa mikutano wa kilele , mazungmzo haya yamekusanya njia za kuimarisha kati ya nchi hizo mbili katika nyanja mbalimbali na kufikia ushirikiano baina ya nchi za Bonde la Mto nile.

Tarere 8-5-2018,Rais wa Uganda Yoweri Museveni alizuru Misri , na Rais wa Misri Abdel Fattah Al Sisi, alimpokea , kiasi kwambaMarais wawili walifanya mazungumzo kuhusu umuhimu wa mahusiano baina ya nchi hizo mbili na masuala ya kimajimbo yenye umuhimu, aidha wametia saini mikataba kadhaa kati ya Misri na Uganda katika Ikulu ya Al-Itihadiya , hasa umuhimu wa ushirikiano wa pamoja katika nyanja ya kilimo, maeneo ya viwanda , umeme na Nishati mbadala.

pembezoni mwa ziara ya Rais Museveni mjini kairo, tume ya pamoja ya nchi mbili ilikutana na Ujumbe wa Uganda uliojumuisha Mawaziri kadhaa na mikataba kadhaa ilisainiwa, na hasa mkataba wa kuanzisha kituo Busia cha umeme wa Nishati ya jua , kufikia jumla mega watt 4, kinachofadhiliwa na serikali ya Misri mkataba wa kufahamiana ,ili kuanzisha maeneo ya viwanda mkataba wa kufahamiana katika nyanja mbalimbali za kilimo.

na shughuli za tume ya pamoja ya ushirikiano imeshuhudia kikao maalumu cha kongamano la kutenda kati ya nchi hizo mbili pamoja na ushirikiano wa makampuni ya Misri na Uganda , na wamekubali kuhusu kuanzisha baraza la kazi za pamoja.

Tarehe 10-3-2019 , Rais Abdulfattah Alsisi alimpigia simu na Rais Museveni akisisitiza kwamba umuhimu wa mahusiano mazuri yameunganisha Misri na ndugu zao uganda, pia pamoja na umuhimu wa mahusiano na mashauriano na Rais Museveni kuhusu masuala ya Afrika kwa sababu yeye anauzoefu mkubwa wa kusukuma juhudi za kuunganisha kiwango cha bara la Afrika, na pia kuhusu kuimarisha mfumo wa utendaji wa Umoja wa Afrika ,wakati akiwa Rais Alsisi ni kiongozi wa Umoja wa Afrika, hasa kuhusiana na masuala ya amani na usalama na ajenda ya maendeleo katika bara la Afrika.

kwa upande wake , Rais wa Uganda alithamini sana mahusiano ya urafiki na undugu baina ya nchi hizo mbili , akitoa pongezi kwa Misri , raia , na viongozi ,na ni matarajio yake kuwepo upeo upana ili kuendeleza mahusiano na kuwepo muundo wa ushirikiano wa pamoja kati ya Misri na Uganda, na pia kuimarisha hatua ya pamoja ya Afrika , kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu kwa nchi za Afrika na raia wake , na kuendelea malengo mshikamano na ushirikiano wa bara la Afrika kwa viwango vyote.

pia walizungumza kwa njia ya mawasiliano ya simu kuonesha njia za ushirikiano wa maendeleo baina ya nchi za bonde la Mto Nile, ambapo maoni yao yalihusu umuhimu wa kuingia katika mawasiliano mazuri kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano wa kimkakati katika eneo la bonde la Mto Nile.

Katika ngazi nyingine:

Ni pamoja na mikutano na mawasiliano inayoendelea kati ya Marais wa nchi hizo mbili, hasa baada ya mwaka 2014 , kuna ziara nyingi sana kwa ngazi ya Mawaziri na viongozi kati ya nchi hizo mbili , miongoni mwao:

Tarehe 21-2-2019 ,Waziri wa umeme na Nishati mbadala Dk.Mohamed Shaker alikwenda Uganda ili kushiriki» Mkutano wa Mawaziri 14 wa Jumuiya ya Nishati kwa nchi za Afrika Mashariki (EAPP) , ambapo iliwasilishwa hotuba ya Misri kwenye mkutano huo.

Kutoka tarehe 26 na 26 septemba ,Waziri wa maji na umwagiliaji, Dk.mohamed abdel Aaty , alizuru uganda ili kushuhudia shughuli za mwisho wa hatua ya kwanza ya mpango wa kuzuia hatari ya mafuriko katika jimbo la Kisisi Magharibi mwa Uganda.

Tarehe 7-5-2018 , Bright Kanituri Rwamirama Waziri wa nchi na mambo ya mashujaa wa vita alikuja nchini Misri na Jenerali Sedky Sobhy Waziri wa ulinzi alimpokea , pande hizo mbili zilijadili maendeleo na masuala ya kikanda na kimataifa na matokeo yake kwa usalama na utulivu ndani ya bara la Afrika. Masuala kadhaa ya ushirikiano wa pamoja wa kijeshi wa nchi hizo mbili ulijadiliwa, na kunufaika kutokana na uzoefu wa Misri katika Nyanja mbali mbali za kijeshi kwa kutoa huduma bora zaidi kwa mashujaa wa vita na waliojeruhiwa katika vita.

Tarehe 8-8- 2017 , Dk. Mohamed Abdel Aaty Waziri wa maji na umwagiliaji , alizuru Uganda kama jitihada za ushirikiano wa Misri kwa juhudi za utekelezaji wa mradi wa kuzuia hatari ya mafuriko katika Kanda ya kisisi Magharibi mwa Uganda, na alipokelewa na Waziri wa maji na mazingira wa Uganda Sam Shaptoris , na pande mbili zilijadili maswala ya pamoja ya kikanda.

Mwaka 2017/5/2 Waziri wa Mambo ya nje Samih Shukry alifanya ziara nchini Uganda na kupokelewa na Rais wa Uganda Yoweri Museveni, Shukry alimkabidhi ujumbe kutoka kwa Rais Sisi unaokusanya mahusiano ya pande mbili na njia za kukuza mahusiano hayo katika nyanja zote. Pande mbili pia zilijadili masuala kadhaa ya kikanda, hasa hali ya Somlia na pembe ya Afrika kiujumla na ushirikiano wa pande mbili katika nyanja ya kupambana na ugaidi. Ziara hiyo ilikuja ndani ya uratibu unaoendelea na mashauriano katia ya nchi hizo

mbili na kuzumgumzia masuala ya mpango muhimu ambao alioutoa Rais wa Uganda kwa ajili ya kuitisha mkutano wa Maraisi wa nchi za Bonde la Mto Nile ambao utalenga kukurubisha maoni kati ya Misri na Sudani na nchi nyinginezo za Bonde la Mto wa Nile.

- Ziara ya Waziri wa maji wa Uganda kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa kiteknolojia wa vyanzo vya maji mjini Cairo Desemba 2016.
- Ziara ya Waziri wa usalama wa Uganda karika mjini Cairo Novemba 2016.
- Ziara ya ugeni kutoka katika idara ya miradi ya utumishi wa kitaifa ya Misri kuelekea Uganda Octoba 2016.
- Ziara ya Waziri wa Mambo ya kiserekali ikiongozwa na ugeni wa kiserekali na bunge kuelekea Sharmu Sheikh kwa ajili ya kuhudhuria mikutano ya bunge la Afrika Septemba 2016, na kwa ajili ya kushirikiana katika kushirehekea Misri kufika miaka 150 tokea kuanzishwa bunge la Misri.

  Tarehe 26-9-2016 ujumbe kutoka katika kamati ya maswala ya mambo ya nje ya bunge la Uganda ulifanya ziara nchini Misri, kupitia ziara hiyo kulijadiliwa hatua za utekerezaji wa miradi ya pamoja ikiwepo ziara ya ijumbe wa mafundi wa Kimisri kwa ajili ya kujenga kituo cha Nishati ya juwa nchini Uganda ikifadhiliwa na mpango endelevu wa kimisri katika nchi za Bonde la Mto wa Nile. Pia walijadili njia za kuendeleza ushirikiano kati ya nchi mbili, hasa katika mambo yanayohusiana na sekta ya bunge, kupitia nafasi iliokuwa nayo kamati ya maswala ya kiafrika iliyoanzishwa katika bunge jipya la Misri. Ziara ya Rais wa miradi ya utumishi wa kitaifa katika jeshi la Uganda mjini Cairo Julai 2016.

- Ziara ya ujumbe rasmi kutoka wizara ya umeme na idara ya ufundi ya kiarabu kuelekea Uganda septemba 2016.
- Ziara ya Waziri wa Nishati wa Uganda mjini Cairo Agosti 2016.
- Ziara ya Waziri wa maji kuelekea Uganda Julai 2016 kwa ajili ya kuhudhuria mikutano ya balaza la Mawaziri la Mto Nile Julai 2016.

- Ziara ya Waziri wa nchi mambo ya nje wa Uganda nchini Misri Juni 2016.

Kushiriki kwa Waziri wa maendeleo na majimbo na elimu ya juu katika hafla ya kutawazwa Rais Museveni mai 2016.

- Ziara ya Mkurugenzi wa idara ya upelelezi wa mambo ya nje wa Uganda mjini Cairo 2016.
- Ziara ya Waziri wa taifa kwa ajili ya makazi wa Uganda nchini Misri 2016.
- Ziara ya pamoja kuanzia Waziri wa nchi wa fedha wa Uganda na Waziri wa nchi wa Uchumi wa mifugo nchini Misri 2016.
- Ziara ya Waziri wa usalama wa Uganda nchini Misri 2016

Tarehe 17-12-2015 Waziri wa umwagiliaji na Rasimali ya maji alifanya ziara ya nchini Uganda kwa ajili ya kukuza mahusiano ya pande mbili kati ya nchi mbili ambapo alipokutana na Waziri wa kilimo mifugo na uvuvi wa Uganda na pande mbili zilizungumzia uhusiano wa kusaidiana katika nyanja nyingi za kisiasa na Rasilimali ya maji.

- Ziara ya ujumbe wa iMamlaka ya Udhibiti ya Misri nchini Uganda Octoba 2015.

Kuhudhuria Waziri wa maji na mazingira wa Uganda hafla ya ufunguzi wa Mfereji wa Suez Agosti 2015.

Tarehe 3-8-2015 katika mfumo wa kutaka Misri kukuza na kuendeleza mahusiano yake na nchi ya Uganda katika nyanja zote, na kufikia maelewano yanayo hitajika katika upande wa faili la maji ya Mto Nile, Jemes Magume Wakili wa Wizara ya Mambo ya nje wa Uganda alifanya ziara nchini Misri, alipokewa katika ziara hiyo na Waziri wa Mambo ya nje Samih Shukry, ambapo ulifanyika mkutano wa mashauriano wa pande mbili na uligusia hali tmbali mbali za mambo ya ndani, kikanda na kimataifa mahala pakutiliwa umuhimu kwa pamoja kati ya nchi mbili, na pia ulifanyika uchunguzi wa matukio ya mahusiano ya pande mbili.

- Ziara ya Naibu wa Waziri wa ugavi wa Misri kuelekea Uganda Agosti 2015.

Tarehe 30-7-20152 Waziri wa sheria na maswala ya kikatiba wa Jamuhuri ya Uganda Kahanda Utavair alifanya ziara nchini Misri, kupitia ziara hiyo alikutana na Rais Abdulfattah Al sisi.

- Ziara ya Ujumbe wa kiusalama wa Misri kuelekea Uganda Juni 2015.
- Ziara ya Waziri wa mambo ya Nje Samih Shukry na kukutana na Rais wa Uganda mwezi wa mai 2015.

Waziri wa Utalii wa Uganda Dk. Maria Mutagamba alitembelea Misri mwezi wa Aprili 2015 , wakati ambapo alikutana na Waziri wa Utalii wa Misri, na walitia saini mkataba wa makubaliano, ili kushirikiana katika nyanja ya Utalii kati ya nchi hizo mbili.

Ujumbe kutoka kutoka Taasisi ya masomo ya kidiplomasia ya Misri walikwenda Uganda mwezi wa aprili 2015 chini ya uongozi wa mkurugenzi wa Taasisi na hii ni miongoni mwa ziara ya nchi za Bonde la Mto Nile, iliyojumuisha Ethiopia na Kenya.

- Ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda nchini Misri na mkutano wake pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri Sameh Shokry mwezi wa Machi 2015.
- Ziara ya wajumbe wa usimamizi wa idara mwezi wa Februari 2014.

Waziri wa Mambo ya kikanda alishiriki katika sherehe na shughuli za uwekezaji na alikutana na Rais wa Misri Abdulfattah Al-sisi mwezi wa June 2014.

msimamizi mkuu wa serikali ya uganda alikuja kairo Mwezi wa Februari 2015 , alikutana na Mwenyekiti wa Kamisheni wa Usimamizi wa idara , na walitia saini mkataba wa ushirikiano kati ya nchi hizo mbili kuhusu kubadilishana uzoefu wa kielimu na kimafunzo katika nyanja ya kuzuia ufisadi.

Tarehe 15-1-2015 ,Ujumbe kutoka Wizara ya Umwagiliaji iliyoongozwa na Mwenyekiti wa kamati ya kifundi na uendeshaji miradi ya ushirikiano wa kiufundi pamoja na Uganda katika uwanja wa Rasilimali za maji na umwagiliaji, ambapo imekubaliwa juu ya kupanua muda rizuku ya Misri iliyotolewa na serikali ya misri kwa serikali

ya Uganda ili kumaliza tatizo la magugu yanayozunguka Mto nchini uganda na pamoja na kukamilika kwa mabwawa ya ukuvuna mvua.

Tarehe 12-1-2015 , Waziri wa maji na Umwagiliaji alikwenda Uganda ili kushiriki mikutano ya kamati ya kiufundi na miongozo ya pamoja kwa ajili ya mradi wa ushirikiano wa kifundi pamoja na Wizara ya maji na Mazingira , Wizara ya Kilimo ,Mifugo ,na Uvuvi ya Uganda.

Waziri wa Fedha wa Uganda na Waziri wa Mifugo walitembelea kairo mwezi wa Septemba 2014 kwa ajili ya kuzungumza suala la kuimarisha biashara na Misri.

- Ziara ya Waziri wa Umwagiliaji na Rasilimali za maji alitembelea Uganda mwezi wa tatu 2014.

Tarehe 20-10-2013 ,Waziri wa Mambo ya Nje Nabil Fahmy alitembelea Uganda kuongoza ujumbe wa urafiki na ushirikiano wa kimisri ambao ulihusisha maono ya Misri ya baadaye na kipaumbele unaofanya kwa ushirikiano wa pamoja na nchi za Afrika.

Ujumbe kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Utawala ulitembelea Uganda katika kipindi cha tarehe 20-27 Mwezi wa sita mwaka 2010.

na katika kipindi cha 24 -31 mwezi wa kwanza mwaka 2010 , Mwenyekiti wa Bunge la watu wa Uganda alitembelea Ofisi ya Mwenyekiti wa Shirika la Mkutano wa Kiislamu , na kuchukua Uenyekiti kwa Uganda.

Sura ya Tatu

Mahusiano ya kiuchumi na kibiashara

Kuna nyanja nyingi na fursa za ushirikiano wa kiuchumi kati ya Misri na Uganda, na pande zake muhimu zaidi ni katika uwanja wa ushirikiano wa maendeleo, mafunzo na kujenga uwezo, hasa kupitia Mfuko wa Misri kwa Ushirikiano wa kiufundi kwa Afrika, ulioanzishwa mwaka 1980, ambao umefanya shughuli zaidi katika uwanja wa ushirikiano kati ya Misri na Uganda kwa miaka 34, na baadaye ulibadilishwa na kuwa Shirikisho la Misri la Ushirikiano kwa ajili ya Maendeleo, ambalo lilianzishwa Julai 1, 2014 baada ya Mfuko wa Misri kwa Ushirikiano wa kiufundi pamoja na Afrika uliunganishwa na Mfuko wa Misri kwa Ushirikiano wa Kiufundi pamoja na Nchi za Jumuiya ya Umoja wa Mataifa, nchi za kiislamu na nchi zilizopata uhuru wake hivi karibuni katika taasisi mpya ambayo ina jukumu la kutoa msaada wa kiufundi na msaada wa kibinadamu kwa ajili ya nchi za Afrika, kuratibu kozi za mafunzo na warsha, kuimarisha ushirikiano pamoja na Umoja wa Mataifa, nchi zilizoendelea, mashirika ya kimataifa na ya kikanda katika mfumo wa ushirikiano (Kusini / Kusini), na aidha ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea na kuchangia kufadhili na kukusanya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Shirikisho la Misri la Ushirikiano wa Maendeleo ni mojawapo ya zana bora zaidi ili kuimarisha mahusiano pamoja na Uganda kwa sababu ya ushirikiano wake katika nyanja mbalimbali, hasa katika maeneo ya mafunzo, kupeleka wataalamu na kujenga uwezo katika nyanja mbalimbali kama : (Polisi, Ulinzi, Mahakama, Kilimo, Maji, Umwagiliaji, Nishati, Afya, Diplomasia na vyombo vya habari) na pia kozi zinazotolewa na Jeshi na Kituo cha Kimataifa cha Misri cha Kilimo, Wizara ya Umeme, Kituo cha Kairo cha mafunzo ya kutatua Migogoro na Uhifadhi wa Amani barani Afrika, Taasisi ya Utafiti wa Polisi na Taasisi ya Mafunzo ya waandishi wa Habari wa Afrika,

ambapo Uganda inachukua nafasi ya kwanza katika nchi za Kiafrika zinazopokea udhamini wa kozi ya Misri, pia katika miaka ya hivi karibuni imeonesha shughuli wazi katika uwanja wa mafunzo kati ya Misri na Uganda, ambapo Misri ilipokea mamia ya wanafunzi wa Uganda katika nyanja mbalimbali kwa kushirikiana na shirika hilo na wadau wote, na matokeo ya kozi hizi yalichangia kudhihirisha mambo mazuri, pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili.

Uwekezaji

Kuna makampuni mengi ya kimisri yanayofanyakazi nchini Uganda, na mengi ya uwekezaji wa kimisri katika maeneo mengi, na makampuni maarufu zaidi ya kimisri ambayo yanafanya kazi kubwa katika soko la Uganda:

- Kampuni ya Mkandarasi wa Kiarabu, ambayo inatekeleza miradi ya miundombinu kwa mikopo ya benki za kigeni kwa ajili ya serikali ya Uganda.
- Kampuni ya Mantrac inayomilikiwa na Mansour Group of Companies.
- Wakili wa Kampuni ya Mac east Africa ya Makampuni ya Mansour.
- Kampuni ya Innovative Research and Development kwa ajili ya udhibiti wa Malaria.
- Kampuni ya Evergreen kwa ajili ya Usafirishaji.
- Kampuni ya Citadel Holding ina 51% ya Kampuni ya Reli ya RVT, ambayo inaunganisha bandari ya Mombasa na Kampala.
- Kampuni ya Washauri wa Kiarabu, Moharram Bakhoum.
- Kampuni ya Wadi Degla imefungua tawi huko Kampala na inafanya kazi katika uwanja wa majengo na miundombinu ya mawasiliano.
- Kampuni ya Misri na Uganda kwa ajili ya Usalama wa Chakula, ambayo ilifunguliwa mwezi Agosti 2016, ni mashine ya kisasa zaidi katika Afrika Mashariki kwa uwekezaji inaofikia dola milioni 10.5, pamoja na baadhi ya miradi ya uwekezaji wa kilimo na mifugo, ambao unamvutia sana Rais Museveni.

- Uuzaji wa kwanza wa nyama ya Uganda kwenda Misri ulifikia tani 50 katika kipindi cha Agosti 2018.
- Kampuni ya Ndege ya Misri.
- Benki ya Kimataifa ya Kairo – Tawi la Kampala
- Kampuni ya Bwawa la Juu kwa Miradi ya Umeme, moja ya makampuni ya sekta ya shughuli za umma, inafanya kazi katika miradi kadhaa ili kuanzisha laini ya chini na ya kati ya voltage kwa ajili ya Mamlaka ya Umeme ya mashamba ya Uganda, na Miradi kadhaa imetekelezwa katika mikoa kadhaa ya Uganda wakati wa 2010.
- Kampuni ya Al-Suwaidi inafanya tafiti za ufanisi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vitatu nchini Uganda (mita za umeme, nyaya, vihami) mbali na eneo la viwanda na kuingia katika zabuni kwa ajili ya kuanzishwa kwa mitandao ya usambazaji na uhamiaji wa umeme kwa ajili ya uwekezaji hadi dola milioni 300.
- Kampuni ya El Nasr kwa kuagiza na kusafirisha imefanya kazi nchini Uganda tangu 1984 na sasa hivi inafanyakazi katika kuhifadhi bidhaa za dawa, vipodozi na vifaa vya umeme, na Kampuni hiyo inafanya shughuli za kuagiza, kuhifadhi na usambazaji kwa jina lake.

Kuna fursa nyingi za uwekezaji nchini Uganda, muhimu zaidi zake ni uwekezaji wa kilimo, kilimo cha viwanda cha mananasi, matunda na kahawa, pamoja na uwekezaji katika sekta ya umeme, ambayo inakabiliwa na uhaba mkubwa pamoja na viwanda kadhaa ambayo inaweza kuwa maarufu sana kama keramik, marumaru, bidhaa za usafi na wengine.

kubadilishana biashara

Kubadilisha biashara kati ya Misri na Uganda bado ni kiwango kidogo, licha ya mahusiano mazuri kati ya nchi hizo mbili, na jitihada za serikali hizo mbili, na licha ya uanachama wa nchi mbili katika vikundi kadhaa na mashirika ambayo huwezesha kubadilishana biashara, na kuna matumaini kwamba eneo la Biashara Huru la Afrika (AFTA),

ambalo limetangazwa kuanzishwa kwake huko Niger mnamo 7/7/2019, ili kuhamasisha biashara ya kubadilishana.

Mauzo ya Misri kwenda Uganda wakati wa 2017 yalifikia dola milioni 38 (kulingana na makadirio ya Chama cha Biashara cha Misri), wakati kiasi cha uagizaji kilikuwa karibu dola milioni 2 tu, ikibainisha hali ya mauzo ya Misri iliongezeka kwa miaka michache iliyopita, kufikia Milioni 44 mwaka 2010 kisha dola milioni 61 mwaka 2013, lakini baadaye ilipungua kiasi, kwani ilifikia dola milioni 54 mwaka wa 2015, kisha katika Mwaka wa 2017 ilipungua hadi milioni 38 tu, wakati mauzo ya Uganda bado ni madogo sana.

Mauzo ya nje ya Uganda yapo katika malighafi kama kahawa na baadhi ya mbegu za matunda, mboga na tumbaku, wakati mauzo ya Misri yanatofautiana ambapo ni pamoja na matunda, baadhi za vyakula, mafuta, dawa na baadhi ya vipodozi. Orodha hiyo pia inajumuisha bidhaa za viwanda kama vile vifaa vya usafi, vifaa vya ujenzi, karatasi, nguo, keramik, Vifaa vya viwandani na vyombo vya umeme.

Kuna uwanja mkubwa mbele ya bidhaa za Misri katika soko la Uganda, hasa kwa wajumbe wa nchi mbili katika COMESA, pia kuna haja ya kuongeza uagizaji mara mbili kutoka Uganda, hususan nyama, chai na kahawa, ili kukuza maslahi ya pamoja.

Mikataba ya Ushirikiano

Misri na Uganda zina makubaliano kadhaa ya ushirikiano katika nyanja mbalimbali. Mikataba ya hivi karibuni ilisainiwa wakati wa ziara ya Rais Museveni nchini Misri mwezi Mei 2018, ambapo ilishuhudiwa na Rais Abdel Fattah Al-Sisi kwa kutia saini makubaliano kadhaa kama:

Mkataba wa taarifa ya mwisho ya kamati ya pamoja kati ya Misri na Uganda, iliyosainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje Sameh Shukri na upande wa Uganda Waziri wa Mambo ya Nje.

Mkataba wa nchi mbili kati ya Wizara ya Umeme na Nishati Mbadala ili kutekeleza kituo cha ualishaji umeme kwa kutumia seli za volta nchini Uganda, na kwa upande wa Misri, Dk Mohamed Shaker, Waziri wa Umeme na Nishati, alitia saini na kwa upande wa Uganda ni Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini ya Uganda.

Mkataba wa utendaji kati ya Wizara ya Umeme na Nishati ya Misri na Nishati na Maendeleo ya Madini nchini Uganda kwa ajili ya kuanzishwa Kituo cha uzalishaji umeme, na kutoka upande wa Misri ulisainiwa na Dr Mohamed Shaker, Waziri wa Umeme na Nishati.

Mkataba wa uelewano katika uwanja wa kuanzisha maeneo ya viwanda kati ya Mamlaka ya Maendeleo ya Viwanda ya Misri na ya Uganda, iliyosainiwa kwa upande wa Misri na Waziri wa Biashara na Viwanda (Tarek Qabeel).

- Mkataba wa ufahamu kati ya Misri na Uganda katika mashamba mbalimbali ya kilimo, ambapo alisaini kutoka Misri, Dk Abdel Moneim El Banna, Waziri wa Kilimo.

Sura ya nne

Ushirikiano kati ya Misri na Uganda kuhusu maji ya Mto Nile

Misri na Uganda ni miongoni mwa nchi za Bonde la Mto Nile. Misri ni nchi ya mwisho wa mto, na Uganda ni nchi ya chanzo cha Mto Nile ambapo vyanzo vyake huko Genja na Ziwa Victoria vinaanza, kwa hivyo ushirikiano kati yao ni jambo muhimu katika maswala ya ushirikiano wa kiufundi juu ya maji ya Mto Nile au kubadilishana uzoefu «ujuzi « kuhusu usimamizi na maendeleo ya rasilimali za maji kwa ujumla.

Kwa hivyo, ipo mifumo ya kisheria, udhibiti na kiufundi kati ya nchi hizo mbili katika uwanja wa maji, na miongoni mwa mifumo hii:

Mkataba wa mwaka wa1953 kati ya Misri na Uingereza kwa niaba ya Uganda kuhusu kuanzisha Bwawa la Owen sehemu ya kutokea Ziwa Victoria. Na mkataba huu mfululizo wa barua nyingi walizotumiana mnamo mwaka wa 1949 hadi 1953 kati ya serikali mbili ya Misri na Uingereza . Na miongoni mwa mambo muhimu zaidi ya mkataba huu; kuashiria kwa Mkataba wa 1929 na kuahidi kuutekeleza mkataba huu unaosema kuwa makubaliano ya kujenga Bwawa la Owen utakuwa kwa mujibu wa Mkataba wa 1929. Uingereza iliahidi katika Mkataba huu kwa niaba ya Uganda kuanzisha na kuendesha kituo cha kuzalisha umeme ambacho hakitahusisha kupunguza kiwango cha maji yanayofika Misri, au kurekebisha tarehe ya kufikia kwake au kupunguza kiwango chake ,jambo linalosababisha madhara kwa maslahi ya Misri.

Mkataba wa mwaka wa 1991 kati ya Misri na Uganda, ambao Marais wa nchi mbili wametia saini na maandiko yake muhimu zaidi ni : « Uganda kuthibitisha kuheshimu Mkataba wa mwaka 1993 ambao Uingereza iliutia saini kwa niaba yake «jambo linalozingatiwa kuwa ni utambuzi wa Mkataba wa 1929. Mkataba huo umeeleza kuwa «Sera za

udhibiti wa Maji ya Ziwa Victoria lazima kujadiliwa kati ya Misri na Uganda kwa mujibu ya mipaka ya usalama bila ya kuathiri mahitaji ya maji ya Misri.» Pia kuna ujumbe wa Umwagiliaji wa kimisri nchini Uganda tangu mwaka wa 1954, ambao kazi yake ya msingi huhusisha na ushirikiano wa kiufundi kuhusu uendeshaji wa bwawa la Owen, pamoja na usimamizi wa utekeleza wa mradi wa Misri na Uganda ili kuondoa magugu na kusafisha mifereji ya maji mbali na maswala kadhaa ya pamoja ya maji.

Misri na Uganda daima zilikuwa na ushirikiano wa pamoja kuhusu maji ya MtoNile, na ushirikiano wa kikanda kati ya nchi za bonde la Mto Nile ulianza mwaka 1967 ambapo walikubaliana kuanzisha mradi kwa ajili ya masomo ya hydrological kwa bonde maziwa ya kitropiki, kamati maalumu ya mradi na wahusika wa kiufundi ni kutoka Misri, Sudan, Kenya, Uganda na Tanzania baadaye Rwanda, Burundi na Zaire, na Ethiopia zilijiunga kama waangalizi, na mradi huo ulitekelezwa na Mpango wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la kimataifa la hali ya hewa (WMO) kwa lengo la kukusanya na kuchambua data ya Hydrometeorology ya maziwa Victoria,Kyoga na Albert, na hivyo ili kuwezesha utafiti wa mizani ya maji kwa Mto Nile, na kazi ya mradi huu ulidumu kwa miaka 25.

Wakati wa kufanyika kwa mkutano wa Mawaziri wa kwanza kwa Baraza la Mawaziri wa Rasilimali za Maji wa nchi za bonde la Mto Nile huko Kampala mnamo mwezi wa Desemba 1992, iliamuliwa kugeuzwa mradi wa maziwa ya kitropiki (mradi wa masomo ya Hydrological kwa mradi wa ushirikiano wa kiufundi wa maendeleo na ulinzi wa mazingira wa bonde la Mto Nile (Tikons), kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya nchi za Bonde la Mto Nile kwa kuendeleza Mradi huu ili uwe taasisi inayojumuisha nchi wanachama zote na iliamuliwa kuunda tume inayojumaisha wajuzi watatu kwa kila nchi ili watoe mapendekezo kuhusu kuanzisha mfumo wa kiushirikiano wa nchi za bonde la Mto Nile.

Na miongoni mwa mifano ya pamoja ya kisasa wa ushirikiano kati ya nchi mbili kuhusu maji ya Mto Nile «Mpango wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni kwa kufanyika Mkutano kwa Marais na Viongozi wa nchi za bonde la Mto Nile huko Entebbe mnano mwezi wa juni 2017 kwa kuzingatia kuwa Uganda inaongoza baraza hili na nchi hizi zimekubali.

Na Mkutano ulifanyaka siku ya juni 22 kwa ushirikiano wa

Mawaziri wa nchi hizi katika ngazi ya nchi mbili, ushirikiano wa Misri na Uganda umeendelea katika nyanja nyingi za maji, kama vile kuchimba visima, ulinzi kutokana na mafuriko, kusafisha maji, kushughulikia maziwa , na mengine. Na miongoni mwa mifano ya miradi ya ushirikiano ya sasa katika swala hili ni kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa kuzuia hatari za mafuriko huku jimbo la Kasisi, Magharibi mwa Uganda.

Wakati wa sherehe ya kuanzisha awamu hii, Waziri Sam Sheptoris ambaye ni Waziri wa Maji wa Uganda, alisifu moyo wa ushirikiano kati ya ndugu huko Misri na Uganda, juhudi za serikali ya Misri zilizowakilishwa katika Wizara ya Rasilimali za Maji na Umwagiliaji kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa rasilimali na umwagiliaji nchini, kukua na kujenga uwezo wa wafanyakazi katika uwanja huu ,vile vile ujuzi mkubwa wa Misri ya kuepuka mafuriko na kuwaepusha Waganda na hatari zake ambazo zimeashiria leo kusherehekea mwisho wa awamu ya kwanza ya mradi huu.

Kwa upande wake, Mkuu wa mkoa wa Kasisi alionesha shukrani kwa Waziri wa Umwagiliaji na serikali ya Misri juu ya juhudi zao za ulinzi kuepuka hatari za mafuriko.

Dk Mohamed Abdel Atty Waziri wa Umwagiliaji alisisitiza kuendeleza ushirikiano wa kiufundi pamoja na upande wa Uganda, kuanza maandalizi kwa ajili ya awamu ya pili ya mradi huo, vile vile kuanzisha mabwawa matano ya kuvuna maji ya mvua katika maeneo mbalimbali ya Uganda, mbali na yale yaliyotekelezwa kutokana na miradi ya visima ili kudhamini upatikanaji wa maji safi ya kunywa kwa wananchi wa Uganda.

Ni muhimu kutambua kwamba mradi wa kuzuia hatari ya mafuriko kwa jimbo la Cassese, magharibi mwa Uganda, unakuja katika mfumo wa ushirikiano wa kiufundi kati ya nchi hizo mbili na kwa ombi la serikali ya Uganda, ili kutoa msaada kupitia uzoefu wa Misri, baada ya hatari inayoshuhudiwa kwa jimbo la Cassese kwa miaka 20, kutokana na mfululizo wa mafuriko, na mafuriko makubwa zaidi yalikuwa mwaka 2014.

Waziri wa Umwagiliaji alibainisha kuwa mkataba wa maelewano wa mradi ulisainiwa kati ya Wizara ya Rasilimali za Maji na Umwagiliaji ya Misri na Wizara ya Maji na Mazingira ya Uganda mwezi Aprili 2016. Na mradi huo unatekelezwa katika hatua kadhaa na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo ilipewa moja ya kampuni kubwa zaidi ya kimisri inayofanya kazi nchini Uganda, kampuni ya Arab Contractors. Awamu ya kwanza ya mradi ni pamoja na utekelezaji wa

kazi za kusafisha juu ya Mto wa Nyamoamba, katika jimbo la Cassese na utekelezaji wa ulinzi kwa kutumia kuta za Japionia katika maeneo manne muhimu kando ya Mto ili kuwalinda kutokana na hatari ya mafuriko yenye uharibifu.

Awamu ya kwanza ya mradi ilianza kutekelezwa tarehe 13/3/2017 kwa moja ya makampuni makubwa ya kitaifa ya Misri. Kazi zilizofanywa ni pamoja na kazi za kuchimba na kusafisha kando ya mto, kuvunja miamba mikubwa na kuiondoa kutoka kwenye mto, ambapo kazi zote za kuchimba na kusafisha zilikamilishwa kando ya Mto mzima wa Nyamumba na kuwasilishwa upande wa Uganda. Na pia ulinzi wa Mto wa Nyamumba ulikamilishwa kwa maeneo yaliyochaguliwa, na awamu ya kwanza ya mradi ilikamilishwa Februari 2018.

Kabla ya ziara ya Waziri wa Umwagiliaji kwenye eneo la mradi katika jimbo la Kassese, Kamati ya kiufundi ya pamoja ya miradi ya ushirikiano kati ya nchi hizo mbili ilifanya mfululizo wa shughuli za mikutano ya Kamati ya kiufundi ya pamoja kwa mradi wa ushirikiano wa kiufundi kati ya Wizara ya Rasilimali za Maji na Umwagiliaji ya Misri na Wizara ya Maji na Mazingira ya Uganda ili kujadili taratibu za utendaji za mradi huo. Waziri wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji Dkt. Mohamed Abdul Ati na Waziri wa Maji na Mazingira wa Uganda Dkt. Sam Sheptoris walikutana na wajumbe wa kamati za kiufundi na mwongozo kwa miradi ya ushirikiano katika nyanja ya rasilimali za maji kati ya nchi hizo mbili ili kuchunguza matokeo ya mikutano ya kamati hizo.

Wakati wa mkutano huo, Waziri huyo alisisitiza kuwa mikutano hii inakuja ndani ya mfumo wa ushirikiano wa kudumu na unaoendelea kati ya Misri na Uganda na kushauriana ili kufuatilia maendeleo ya kazi katika miradi ya ushirikiano kati ya nchi hizo mbili katika nyanja ya rasilimali ya maji na umwagiliaji, ambao sasa ni mradi wa ushirikiano na Wizara ya Maji na Mazingira ya Uganda, Na mnamo Januari 2010 ulisainiwa mkataba wa kuafikiana ili kutekeleza miradi kadhaa muhimu kwa wananchi wa Uganda kwa udhamini wa Misri wa dola milioni 4.5, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa uchimbaji visima vya maji 75 katika maeneo mbalimbali nchini Uganda ili kuwapatia maji ya kunywa, ambavyo vilikamilishwa mwezi wa Desemba, 2016, na pia ulianza utekelezaji wa mapendekezo ya kuwaelimisha jamii namna ya uendeshaji, matengenezo ya visima na umuhimu wa kuhifadhi visima, pamoja na kumaliza kuleta vifaa vikubwa vinavyotumiwa katika utekelezaji wa miradi yote, na mradi ambao ni muhimu zaidi kuliko yote ni mradi wa kujenga mabwawa ya kukusanya maji ya mvua ili kuhifadhi maji ya kunywa kwa wananchi na matumizi ya nyumbani,

ambapo mkataba wa kutekeleza mradi huo ulisainiwa na kampuni ya Uganda katika mwezi wa Agosti.

Wizara ya Umwagiliaji ya Misri ilitangaza katika maelezo yake, kuanza utekelezaji wa mradi wa kujenga mabwawa matano kwa ajili ya kukusanya maji ya mvua katika maeneo mbalimbali nchini Uganda kwa ukubwa usio zaidi ya meta za kyubiki 10000.

Victoria - Alexandria

Wizara ya Rasilimali ya Maji na Umwagiliaji pia ilitangaza kukaribia kukamilisha masomo ya mradi wa Mto kati ya Ziwa la Victoria na Alexandria, ili kukuza ushirikiano wa kimaendeleo, kiuchumi na kitamaduni kati ya raia wa Afrika na bonde la Mto Nile, ili kuongeza mawasiliano ya kiutamaduni kati ya raia wa Afrika na kurejesha mawasiliano ya kisiasa na kutatua baadhi ya migogoro iliyoachwa na ukoloni kwa baadhi ya nchi . Hata ndani ya baadhi ya nchi kati ya makabila na makundi, na kwamba utekelezaji wa mradi huo utakuwa hatua ya kwanza ya kikanda utajengwa baadaye ili kuwa mwanzo wa hatua nyingine kubwa zaidi juu ya kiwango cha bara.

Misri imepiga hatua kubwa katika utafiti na kwamba ushauri wa kimataifa umewasilishwa ripoti yake kwa kampuni inayotekeleza mradi huo na ilitolewa kwa nchi wanachama. Mradi huo pia upo chini ya usimamizi wa sekretarieti ya NEPAD, moja ya miradi ya kikanda ambayo Misri inatarajia kuwa ni fursa inayofaa kwa nchi za Bonde la Mto Nile ili zikubali na kuanzisha utaratibu wa kikanda ambao utatumiwa katika hatua za baadaye ili kuwa mwanzo kwa hatua nyingine ya kina zaidi juu ya kiwango cha Afrika, ndani ya mfumo wa dhana zilizosisitizwa na Marais na serikali.

Ripoti ya Kamati ya Ushauri ni pamoja na kuanzishwa kwa muundo wa kitaasisi na kisheria kwa mamlaka ya kikanda iliyopendekezwa kusimamia mradi huo, pamoja na kuchangia kwa nchi zote wanachama, na mahitaji ya mafunzo ya lazima, viongozi katika nchi wanachama na njia za kubadilishana uzoefu na taarifa kati ya washiriki.